CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

SUA

SUA YAFAIDIKA MIAKA MITANO YA JPM

"Hakuna Chuo Kikuu chochote nchini cha kuendeleza kilimo, ufugaji na uvuvi isipokuwa SUA pekee, ndiyo maana nimekuja kuwapa hamasa mchape kazi, tembeeni kifua mbele". Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli 07 May, 2018

DIBAJI

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kilianzishwa rasmi mnamo tarehe 01 Julai 1984 kwa Sheria ya Bunge Na. 6 ya mwaka 1984. SUA ilipewa Hati Idhini mwaka 2007 chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya mwaka 2005.

Chuo hiki kinatoa wataalamu kuanzia ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada za Kwanza, Shahada za Umahiri na Shahada za Uzamivu. Watalaamu wanaotolewa na SUA hutoa mchango mkubwa katika ujenzi wa Taifa kupitia huduma yao katika sekta mbalimbali serikalini na zile za kibinafsi. Chuo kimejiwekea malengo ya kimkakati ambayo ni kuongeza udahili wa wanafunzi, miradi ya utafiti na kuboresha huduma za ugani na ushauri wa kitaalamu. Hata hivyo kwa miaka mingi Chuo kilishindwa kufikia malengo hayo kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo uchakavu wa miundombinu na mifumo ya huduma za jamii.

Kupitia Serikali ya Awamu ya Tano, Chuo kimetatua changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga Maabara Mtambuka Kampasi Kuu, Maabara ya Sayansi Solomon Mahlangu, kukarabati viwanja vya michezo, kuanzisha shamba la mafunzo la mfano, kukarabati Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama, kukarabati madarasa na mabweni, kununua mabasi, pamoja na kupanua na kusajili Hospitali ya SUA. Maboresho hayo ya miundombinu yamekifanya Chuo kuongeza programu mpya za masomo 26, kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 9,165 mwaka wa masomo 2015/16 hadi 13,199 mwaka wa masomo 2019/20. Katika kipindi hiki jumla ya wataalamu 13,178 ambao wamehitimu katika program mbalimbali.

Menejimenti ya Chuo inatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Profesa Raphael T. Chibunda
Makamu Mkuu wa Chuo

1.0 UTANGULIZI

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilianzishwa rasmi mnamo tarehe 01 Julai 1984 kwa Sheria ya Bunge Na. 6 ya mwaka 1984. Hata hivyo historia ya Chuo hiki inaanzia mwaka 1965 kilipoanza kama Chuo cha Kilimo kilichokuwa kinatoa mafunzo ya Stashahada (Diploma) ya Kilimo.

Kufuatia kufutwa kwa Chuo Kikuu cha Afrika ya Mashariki kulikopelekea kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Kilimo kilibadilishwa kuwa Kitivo cha Kilimo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia tarehe 01 Julai, 1970.

Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya mwaka 2005 ilifuta Sheria Na. 6 ya mwaka 1984 iliyounda Chuo. Hivyo chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya mwaka 2005, Hati Idhini ya SUA (SUA Charter), 2007 iliandaliwa, kuidhinishwa na kukabidhiwa kwa Chuo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dira

Dira ya Chuo ni kuwa Chuo kiongozi katika taaluma za Kilimo na Sayansi shirikishi.

Dhima

Dhima ya Chuo ni kuchochea kuongeza maendeleo katika nyanja za Kilimo, Maliasili na Sekta Shirikishi kwa njia ya mafunzo, utafiti na kutoa huduma.

Malengo

(i) Kuongeza udahili wa wanafunzi na ubora wa wahitimu
(ii) Kuongeza wingi na ubora wa Tafiti, Machapisho na Uvumbuzi
(iii) Kuboresha utoaji wa huduma za ugani, utangazaji wa Chuo na ushirikiano na Taasisi nyingine
(iv) Kuongeza uwezo endelevu wa Chuo kifedha
(v) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia
(vi) Kuboresha usimamizi na Utawala Bora katika Taasisi
(vii) Kuhusisha Masuala ya Kijinsia katika shughuli zote za Chuo na kupunguza madhara ya Virusi vinavyosababisha maam bukizi ya Ukimwi na mambo mtambuka

Changamoto

(i) Upungufu na uchakavu wa baadhi ya miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kama vile kumbi za mihadhara, maabara, mabweni ya wanafunzi na miundo mbinu mingine. Miundo mbinu mingi ya Chuo iliyopo imejengwa kati ya mwaka 1965 na 1980 ambayo uwezo wake (capacity) kwasasa ni mdogo ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi waliopo. Hii imesabisha pia Chuo kushindwa kupanuka kwa haraka kama inavyoelekezwa kwenye Mpango Mkakati wa Chuo.

(ii) Ubovu wa miundo mbinu ya barabara za ndani ya Chuo

(iii) Ufinyu wa bajeti ya maendeleo na uendeshaji wa Chuo.

(iv) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuendesha Programu za mafunzo kwa wakulima na Maafisa Ugani ikiwa ni pamoja na kusambaza matokeo ya utafiti.

(v) Uwepo wa bajeti ndogo kwa ajili ya utafiti. Kwa muda mrefu sasa shughuli za utafiti karibu asilimia 99.9 zinafadhiliwa na Wadau wa Maendeleo.Hivyo kuna hatari siku za usoni wafadhili watapunguza ufadhili wao kwenye tafiti na kufanya eneo hili kuathirika.

2.0 MAFANIKIO

Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mhe. Dkt John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatimiza Miaka Mitano tangu iingie madarakani. Katika kipindi hiki cha miaka mitano kilichoanzia mwaka 2015 hadi 2020 mambo mengi yamefanyika katika sekta mbalimbali zikiwemo za kilimo, mifugo na uvuvi, afya, utalii, miundombinu, madini, elimu, maji, na nyingine nyingi.

Kwa muda mrefu Sekta hizi zilikuwa zimezorota na kuwa na hali duni sana lakini Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi hiki kifupi imeacha alama chanya katika kila sekta. Mfano ujenzi wa reli ya umeme ya Standard Gauge (SGR), ujenzi na uboreshaji wa Hospitali na Vituo vingi vya Afya, ujenzi wa miundombinu ya barabara, ununuzi wa ndege, ununuzi wa vivuko na meli mpya na kufufua za zamani, ujenzi wa majosho, kuboresha mfumo wa uuzaji na bei za mazao hasa ya kimkakati, ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kufundishia kuanzia ngazi ya shule za Msingi hadi Vyuo Vikuu.

SUA ni miongoni mwa Taasisi za Elimu zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambazo zimefaidika na mambo makubwa yaliyofanyika katika kipindi hiki cha miaka mitano ya Rais John Joseph Pombe Magufuli. Mambo haya yamekiwezesha Chuo kuchangia maendeleo ya nchi hususani kwenye sekta ya elimu sayansi na teknolojia kwenye nyanja za kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na maendeleo vijijini kwa ujumla na kuchangia nchi kuingia kwenye uchumi wa kati.

Katika kipindi cha miaka mitano 2015-2020 Chuo kimeweza kutekeleza ujenzi wa Maabara Mtambuka Kampasi Kuu, ujenzi wa Maabara ya Sayansi Solomon Mahlangu, ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo, uanzishwaji wa shamba la mafunzo la mfano, ukarabati wa Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama, ukarabati wa madarasa na mabweni, ununuzi wa mabasi na upanuzi na usajili wa Hospitali ya SUA.

Inaendelea Uk. 5

Inatoka Uk. 4

Maboresho hayo ya miundombinu yamekifanya Chuo kuongeza programu mpya za masomo 26, kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 9,165 mwaka wa masomo 2015/16 hadi 13,199 mwaka wa masomo 2019/20, na pia kutoa jumla ya wataalamu 13,178 ambao walihitimu katika programu mbalimbali.

Yafuatayo ni mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020;

KUPANUA SHUGHULI ZA CHUO SEHEMU MBALIMBALI NCHINI.

Kwa muda mrefu Chuo kimekuwa kikifanya shughuli zake katika kampasi zake za Morogoro ambazo ni Kampasi Kuu (Hekta 2,376) na Kampasi ya Solomon Mahlangu (Hekta 1,050). Chuo pia kinamiliki vitengo vya mafunzo kwa vitendo vilivyopo Olmotonyi, Arusha na Mazumbai, Tanga ili kuwafikia wakulima na wadau wengine na kusogeza huduma karibu na wananchi. Katika kipindi cha miaka mitano, Chuo kimefanikiwa kuanzisha Kampasi mpya ya Mizengo Pinda katika Kijiji cha Kibaoni, Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, Wilaya ya Mlele Mkoa wa Katavi. Kampasi hiyo ina eneo la ekari 68 lenye majengo takribani 30

pamoja na shamba lenye ukubwa wa ekari 200. Kampasi hiyo inaanza kudahili wanafunzi kwa mwaka huu wa masomo 2020/21.

Katika Kampasi ya Mizengo Pinda, Chuo kinatarajia kudahili wanafunzi 300 katika programu tatu za masomo ambazo ni Shahada ya Awali ya Sayansi ya Usimamizi Rasilimali Nyuki (BSc. Bee Resources Management), Stashahada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mimea Vipando (Diploma in Crop Production and Management) na Astashahada ya Utalii na Shughuli za Uwindaji (Certificate in Tour Guiding and Hunting Operations) kwa mwaka wa masomo 2020/21. Uanzishwaji wa Kampasi hiyo ni jitihada za Chuo katika kuunga mkono malengo na utekelezaji wa sera ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na

wataalamu wa kutosha na kutekeleza adhima ya Tanzania kufikia uchumi wa viwanda.

Aidha, mnamo mwaka 2018 Chuo pia kimeanzisha kituo cha mafunzo katika eneo la Daraja Mbili Halmashauri ya Wilaya Tunduru Mkoani Ruvuma. Chuo kimetenga eneo hilo ambalo kilipewa na serikali kwa ajili ya shughuli za kitaaluma, utafiti, ugani na kuhudumia jamii ya Tunduru ikiwemo mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaosoma Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Usimamizi wa Wanyamapori.

Vilevile mwaka 2018 SUA ilipewa na serikali eneo la hekta 10,000 katika Kijiji cha Ifinga, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba Mkoani Ruvuma kwa ajili ya kuanzisha Msitu wa mafunzo wa kibiashara, utafiti na ugani na tayari SUA imepanda miti takribani hekta 800 katika eneo hilo.

2.1 MAFANIKIO YA KITAALUMA

KUONGEZEKA KWA PROGRAMU MPYA ZA MASOMO (MITAALA)

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa muda mrefu hakikufanikiwa kuongeza idadi ya programu za muda mrefu na muda mfupi kutokana na upungufu wa miundombinu ya kufundishia kwa nadharia na vitendo ambapo mwaka 2013/14 Chuo kilikuwa na jumla ya Programu 97. Aidha kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Chuo kimeongeza programu mpya za masomo 26 ambazo ni; shahada za uzamili 17, Shahada za Awali 7, stashahada 1 na astashahada 1. Pia Chuo kimeanzisha shahada 4 za uzamivu zinazotolewa kwa njia ya tamrini "Thesis" na tasnifu "Dissertation".

Kwa sasa SUA ina jumla ya program 116 ambazo ni Stashahada za uzamili 3, Shahada za Juu 69, Shahada za Awali 36, Stashahada 6, na Astashahada 2. Mafunzo yanayotolewa yamejikita katika maeneo ya Kilimo (utaalamu wa vipando, uzalishaji mazao, uhandisi kilimo na uhandisi umwagiliaji, usindikaji wa mazao kilimo na chakula na lishe ya binadamu, ugani na elimu ya jamii); Mifugo (Tiba ya Mifugo, Baioteknolojia na Maabara, uzalishaji wanyama, ufugaji samaki; nyanda za malisho) Kilimo-biashara; Misitu na Wanyamapori (upandaji na utunzaji misitu, wanyamapori na utalii); Sayansi na Elimu (Utunzaji mazingira; ualimu wa masomo ya sayansi ikiwemo Hisabati, Baiolojia, Kemia, Fizikia, Jiografia na Kilimo); na maendeleo vijijini. Program hizi zinachangia moja kwa moja kukuza uchumi wa viwanda.

KUONGEZEKA KWA IDADI YA WANAFUNZI (UDAHILI)

Kwa muda mrefu SUA imekuwa ikipokea maombi mengi ya wanafunzi wanaotaka kujiunga na kozi mbalimbali. Hata hivyo changamoto kama mitaala michache pamoja na hali mbaya ya miundombinu ziliathiri uwezo wa Chuo kudahili idadi kubwa ya wanafunzi.

Chuo kimeongeza udahili wa wanafunzi wa shahada za awali kutoka 9,165 mwaka wa masomo 2015/16 hadi kufikia wanafunzi 13,199 Mwaka wa masomo 2019/20. Kati ya hao kuna wanafunzi wa kigeni 76 kutoka nchi mbalimbali. Pia, kumekuwa na ongezeko la wahitimu kutoka 2,317 mwaka wa masomo 2015/16 hadi kufikia wahitimu 2,882 mwaka wa masomo 2018/19 na matarajio ni wahitimu 3,400 kwa mwaka wa masomo 2019/2020.

Mwaka 2015 Chuo kilikuwa na jumla ya matrekta 7 na mengi ya matrekta hayo hayakuwa katika hali nzuri kuweza kutumiwa kwa mafunzo na hivyo kuleta changamoto katika mafunzo kwa vitendo.

Kwa kutambua mchango wa SUA kwenye sekta ya Kilimo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alipotembelea Chuo Kikuu cha Sokoine mnamo tarehe 7 Mei, 2018 alikipatia Chuo Matrekta 10 aina ya URSUS pamoja na

Inaendelea Uk.9

Inatoka Uk. 8

vifaa vyake (Majembe 8 na Harrow 2) vyenye thamani ya shilingi milioni 587.5 kwa ajili ya kuboresha shughuli za mafunzo na uzalishaji mali chuoni. Akiahidi kutoa Matrekta hayo Mheshimiwa Rais alisema; "Hakuna Chuo Kikuu chochote nchini cha kuendeleza kilimo, ufugaji na uvuvi isipokuwa SUA pekee, ndiyo maana nimekuja kuwapa hamasa mchape kazi, tembeeni kifua mbele. Leo nilitakiwa niwe nimeshaondoka Morogoro lakini nikasema siwezi kuondoka mpaka nikutane na ndugu zangu wanaosoma na wanaofanya kazi Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo".

Upatikanaji wa matrekta haya kwa kiasi kikubwa umesaidia na unaendelea kusaidia kuimarisha ufundishaji kwa vitendo na kuongeza uzalishaji kama ilivyokuwa matamanio ya Mhe.Rais.

Picha kubwa ni muonekano wa jipya kati ya kumi yaliyotolewa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli alipotembelea SUA na picha ndogo ni muonekano wa Trekta la zamani

UJENZI NA UKARABATI WA MAABARA NA MADARASA

Ufinyu wa madarasa na maabara kwa muda mrefu umekuwa ni changamoto kubwa katika kuhudumia wanafunzi kwa wakati mmoja ukizingatia baadhi ya kozi zina wanafunzi wengi jambo ambalo lilipelekea wanafunzi kuingia kwa zamu na wengine kutoka wakati wa usiku na kuhatarisha usalama wa wanafunzi hao. Yafuatayo yamefanyika katika kipindi cha mwaka 2015-2020 katika kuboresha maeneo hayo kwa kuzingatia ongezeko la wanafunzi:

Ujenzi wa Maabara Mtambuka-Kampasi Kuu

Chuo kimejenga jengo la Maabara Mtambuka kwa gharama ya shilingi Bilioni 11.4. Jengo hili lina maabara nane (8) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kwa wakati mmoja na madarasa nane (8) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kwa ujumla. Pia litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2400 kwa wakati mmoja na litajumuisha, Ofisi saba zitakazoweza kutumika kwa wafanyakazi 38, vyumba vya maandalizi 11; Stoo 7 kwa ajili ya kuhifadhia kemikali. Fedha zinazotumika katika ujenzi wa Maabara ni za Serikali.

Jiwe la msingi la maabara hiyo liliwekwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 7 Agosti, 2019.

Muonekano wa Maabara Mtambuka iliyopo Kampasi Kuu SUA

Ujenzi wa Maabara ya Sayansi Kampasi ya Solomon Mahlangu

Chuo kimekamilisha ujenzi wa Maabara ya Sayansi katika Kampasi ya Solomon Mahlangu kwa ufadhili wa Serikali ya Kifalme ya Norway. Ujenzi wa maabara hiyo umegharimu kiasi cha shilingi Bilioni 2.6. Jengo hilo lenye maabara 4 zenye uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 100 kwa kila maabara na hivyo kuhudumia wanafunzi 400 kwa wakati mmoja kwa kiasi kikubwa limetatua changamoto kubwa ya maeneo ya kufanyia mafunzo kwa vitendo.

Muonekano wa Maabara mpya ya Sayansi ya Solomon Mahlangu. Picha chini (kushoto) ni muonekano wa ndani wa maabara ya zamani na (kulia) ni muonekano wa ndani wa maabara ya sasa

Ununuzi wa vifaa vya Maabara ya udongo

Katika kipindi cha mwaka 2015-2020 chuo kimenufaika na mpango wa Serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kuboresha miundombinu ya maabara ya udongo, kwa kupata fedha kiasi cha shilingi Milioni 400 zilizowezesha kununua vifaa vipya na vya kisasa. Vifaa hivyo ni pamoja na Inductively Coupled Plasma Optic Emission Spectroscopy (ICP OES), Multiwave digester, na matengenezo ya vifaa vingine vya maabara. Kupitia mpango huu, Serikali imewezesha kuinua kiwango cha mafunzo kwa vitendo katika ngazi za shahada za awali na uzamili, ubora wa tafiti mbalimbali za kilimo zinazohitaji maabara hii, kutoa huduma kwa wakulima na wawekezaji katika kilimo, na kupunguza kwa kiasi kikubwa ulazima wa kusafirisha sampuli nje ya nchi kwa ajili ya kuchunguza udongo na mimea. Kwa sasa maabara ya udongo imeweza kuongeza ufanisi na kuchakata sampuli 4000 kwa mwaka kutoka kwa wadau mbalimbali, ikiwemo wakulima wadogo, makampuni ya kilimo na watafiti wa SUA na tasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mwanafunzi akiwa kwenye Maabara ya Sayansi ya Udongo iliyopo Kampasi Kuu SUA

Wataalamu wa Maabara wakiwa nje ya Jengo la Maabara ya Sayansi ya Udongo

Ukarabati wa Maabara za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Katika kipindi cha mwaka 2015-2020 Chuo kimekarabati maabara tano za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano zilizopo Kampasi Kuu na Kampasi ya Solomon Mahlangu kwa gharama ya Dola za Kimarekani Milioni 2.5 kuziwekea vifaa vya kisasa zikiwemo Kompyuta 484. Fedha za ukarabati wa maabara hizo zilitolewa na mradi wa ESUA-CICT uliofadhiliwa kupitia Shirika la USAID la Serikali ya Marekani iliyoshirikiana na Serikali ya Tanzania. Maabara hizo zimesaidia kuboresha ufundishaji wa masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Picha kubwa na ndogo ni muonekano wa ndani wa vyumba vya Maabara za Teknoojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Ujenzi na Ukarabati wa madarasa

Katika kipindi cha mwaka 2015-2020 chuo kwa kushirikiana na Serikali ya Awamu ya Tano kimefanikiwa kukarabati madarasa matatu (3). Madarasa hayo yanahusisha kujenga madarasa ya wanafunzi wa Shahada za uzamili na shahada za awali kwa lengo la kuongeza nafasi za maeneo ya kufundishia na kujifunzia. Ukarabati huu umehusisha kubadili matumizi ya baadhi ya majengo yaliyokuwa yanatumika kwa kazi nyingine kama vile kuhifadhia chakula cha mifugo na kulifanya kuwa darasa na kuongeza nafasi za kujifunzia. Ukarabati huo ume-ongeza nafasi 300 za kukaa wanafunzi kwa wakati mmoja. Ukarabati huu umegharimu kiasi cha shilingi Milioni 22.3.

Picha juu zikionesha jengo la HAY lililobadilishwa na kuwa darasa na picha ya chini kulia ni jengo la darasa lililokarabatiwa kwenye Idara ya Uhandisi Kilimo

UJENZI NA UKARABATI WA KARAKANA NA KIWANDA CHA SAMANI

Muonekano wa Kiwanda cha Samani (Vuyisile) baada ya kufanyiwa ukarabati

Idara ya Uhandisi Kilimo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimoni moja ya Idara kongwe na imefanikiwa kutoa wahandisi Kilimo wengi sana lakini kwa mda mrefu Idara hii imekuwa na miundombinu duni ya kufundishia.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Chuo kilipata shilingi milioni 750 kwa ajili ya ukarabati wa karakana za uhandisi kilimo. Fedha hizo zilitolewa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Chuo kinatumia fedha hizo kufanya ukarabati wa karakana 5 za uhandisi kilimo na ukarabati wa kiwanda cha kutengeneza samani cha Vuyisile. Karakana hizo zitasaidia wanafunzi wanaosoma programu za misitu na uhandisi kilimo kujifunza kwa vitendo utengenezaji wa zana na bidhaa mbalimbali za misitu na kilimo. Karakana zilizokuwepo hapo mwanzo majengo yake yalikuwa yamechakaa na vifaa vingi vilikuwa havifanyi kazi na hivyo kusababisha changamoto ya utoaji mafunzo na ufanyaji wa tafiti husika.

Picha juu ni muonekano wa Jengo la Karakana ya Uhandisi Kilimo ambalo limefanyiwa ukarabati na picha chini ni muonekano wa jengo la Uhandisi Kilimo ambalo lipo kwenye hatua za mwisho za ujenzi

UKARABATI HOSPITALI YA TAIFA YA RUFAA YA WANYAMA

Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama iliyopo katika Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya ilipewa heshima ya kuwa Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama kwa nchi nzima. Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani Hospitali hiyo imekuwa na mchango katika kuboresha afya za Wanyama. Hospitali hiyo ilikuwa haijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu na vifaa muhimu vya hospitali hiyo vilikuwa vimechakaa na vingine kuharibika.

Kwa kutambua hilo na kupitia msaada wa serikali Chuo kimeendelea kuboresha Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama kwa kufanya ukarabati mkubwa wa majengo na kununua vifaa tiba. Baadhi ya vifaa tiba vilivyonunuliwa ni pamoja na "Computed Radiography Reader Machine" kwa ajili ya kusafishia picha za "X-ray" za kidijitali na mashine ya usingizi "Anaesthetic Machine" kwa ajili ya kutolea ganzi kwa wanyama kwa gharama za shilingi Milioni 100. Hospitali hiyo pia hutumika kufundishia wanafunzi wa Shahada ya Tiba ya Mifugo, utafiti na ushauri wa kitaalamu. Ukarabati na ununuzi wa vifaa umesaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha huduma zinazotolewa na hospitali hiyo. Hii ndio hospitali pekee ya rufaa nchini kwa ajili matibabu ya mifugo na wanyama wengine.

Wanafunzi wakiwa kwenye chumba cha matibabu ya wanyama cha Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya wanyama

Muonekano wa nje wa Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya wanyama inayoendelea kukarabatiwa

UANZISHWAJI WA SHAMBA DARASA LA MFANO

Kwa muda mrefu hali ya mashamba ya mafunzo ya Chuo ilikuwa hairidhishi kwa kiasi kikubwa, kulikuwa na miundombinu na vifaa vilivyopitwa na wakati na chakavu hivyo kuathiri utoaji wa elimu kwa vitendo.

Kupitia jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo elimu ya Juu, Chuo kimeanzisha shamba darasa la mfano (University Training Model Farm) kwa madhumuni ya kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo. Uimarishaji wa mashamba darasa unalenga kuwapa wanafunzi fursa nzuri ya kujifunza kwa vitendo zaidi ili wakihitimu wawe na ubora unaotakiwa sambamba na uwezo wa kwenda kuwa wakulima wa mfano, kushauri na kubadili kilimo cha nchi yetu. Katika shamba hilo Chuo kimepanda mazao ya kimkakati ya kitaifa ili wanafunzi waweze kupata maarifa juu yake. Mazao hayo ni kama vile korosho, alizeti, zabibu, kokoa, miwa, kahawa, chikichi, nazi, chai, katani na pamba pamoja na mazao ya mbogamboga na matunda ikiwemo, mipapai, nanasi, migomba, miembe, mapera, malimao, na mipasheni. Lengo la Chuo ni kuchangia katika kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini na kuongeza pato la taifa kupitia maendeleo ya viwanda vya mazao ya Kilimo.

Muonekano wa shamba darasa la mfano lililopo Kampasi Kuu SUA

Inatoka Uk. 18

Shamba hili linajumuisha shamba la mifugo la magadu lenye jumla ya ekari 105, kitengo/eneo la bustani lenye ukubwa wa ekari 37 pamoja na eneo la mazao mchanganyiko lenye jumla ya ekari 55.

Shamba la mfano linajumuisha vitalu nyumba 6 na makumbusho ya mimea vipando (crop museum) ekari 23 ikijumuisha eneo la hifadhi ya mazao ya kimkakati ya kitaifa.

Picha juu na chini ni eneo la shamba la mifugo lililopo Magadu ambalo majengo yake ya kulishia yapo kwenye ukarabati

Makumbusho ya Mimea Vipando (Crop Museum)

Chuo kimeendelea kufanya maboresho ya eneo la Hifadhi na Makumbusho ya Mimea Vipando (Crop Museum) ili kutunza historia ya mimea na mazao mbalimbali nchini.

Katika makumbusho hayo mazao mbalimbali yamepandwa kwenye eneo la ukubwa wa robo ekari kwa kila zao na kuweka miundombinu ya umwagiliaji ya kisasa kwa njia ya matone na kunyunyiza, kujenga uzio na vitalu nyumba. Serikali ya awamu ya tano imekiongezea nguvu Chuo kwa kuongeza miundombinu mipya ili kukiwezesha kutoa wanafunzi bora wenye weledi na ujuzi mkubwa wa kisayansi na kiteknolojia kuhusu mazao husika. Makumbusho haya pia ni muhimu kwa jamii zinazozunguka SUA na nchi kwa ujumla hususan katika suala pana la ushauri na ugani na kujifunza kwa kujionea baadhi ya mazao ambayo wanaimani yanastawi tu katika maeneo mengine nchini. Hii imesaidia katika kupanua wigo wa wananchi katika kuelewa kilimo cha mazao hayo ya kimkakati kitaifa.

Muonekano wa Vitalu nyumba vilivyopo kwenye Makumbusho ya mimea vipando (Crop Museum)

2.2 MAFANIKIO YA KIUTAFITI

MIRADI MIPYA

Chuo kimekuwa mwenyeji wa miradi mikubwa ya utafiti kama vile

- Kituo cha Taifa cha Uratibu wa Hewa ya Ukaa (NCMC) chenye mradi wenye thamani ya krona za Norway Milioni 37.
- Kituo cha Utafiti wa Magonjwa Ambukizi cha Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (SACIDS) chenye miradi yenye thamani ya dola za Kimarekani Milioni 25.
- Kushinda Vituo viwili vya Umahiri vya Afrika (African Centres of Excellence) kwenye utafiti wa magonjwa ambukizi ya wanyama na binadamu na Teknolojia ya kutumia Panya buku wa kunusa yenye thamani ya dola za Kimarekani Milioni 12; kutatua matatizo ya jamii (kwa kubaini wagonjwa wa kifua kikuu na kubaini mabomu yaliyoteg wa ardhini).
- Vilevile, Chuo ni mwenyeji wa mradi mkubwa ujulikanao kwa jina la REFOREST AFRICA wenye thamani ya dola za kimarekani Milioni 18.
- Chuo pia kimeanzisha Kigoda cha Utafiti chini wa Wakfu wa Utafiti wa Oliver Tambo ambapo kupitia Wakfu huo Chuo kitapata ufadhili wa Dola za Kimarekani Laki 195.3 kila mwaka kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka 2020.

Panya Buku akiwa katika mafunzo ya jinsi ya kutegua mabomu ardhini

MACHAPISHO

Chuo huchapisha wastani wa machapisho ya kitaalamu 500 kwa mwaka kwenye majarida mbalimbali yanayotambulika kitaifa na kimataifa. Hii imetokana na kuongezeka kwa ufadhili na kuboreshwa kwa miundombinu katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

SUA imekuwa na mchango mkubwa sana kupitia tafiti za kisayansi nchini na ulimwenguni. Kwa mfano, kwa matokeo yaliyotolewa na Shirika la "Webometrics" mwezi Julai, 2020, SUA imeshika nafasi ya kwanza kitaifa katika matumizi ya tafiti zake (citation index) ambapo zaidi ya watafiti 82,220 duniani wametumia machapisho ya SUA katika maandiko yao. Mchango huu ni karibia mara mbili zaidi ya vyuo vikuu vilivyoshika nafasi ya pili, ya tatu na ya nne kwa pamoja kitaifa, na nafasi yetu kidunia imepanda kufika nafasi ya 1,161 kati ya vyuo vikuu bora 5,800 duniani. Aidha, nafasi ya SUA kwa ubora wa jumla imepanda hadi kufikia nafasi ya pili kitaifa mwezi Julai, 2020 ukilinganisha na nafasi ya tatu, Mwezi Januari, 2020. Kwa kupitia hizi tafiti Chuo kimesaidia kutatua matatizo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi na masuala ya kuondoa umaskini kwa wananchi.

HATAZA/HATI MILIKI

Chuo kimefanikiwa kupata hataza 12 katika baadhi ya maeneo ya tafiti katika kipindi cha mwaka 2015/2020, kama vile ugunduzi wa mbegu mbalimbali za mazao kama vile mpunga, maharage na uzalishaji wa miche ya matunda kwa njia ya chupa, chanjo na visumbufu vya mazao na mifugo.

Chuo huchapisha wastani wa machapisho ya kitaalamu 500 kwa mwaka kwenye majarida mbalimbali yanayotambulika kitaifa na kimataifa.

Ujenzi wa jengo la kukuzia na kutunzia wadudu na wanyama wadogo waharibifu kwa ajili ya utafiti

Katika awamu hii pia, Chuo kimejenga jengo la Maabara ya Utafiti na Udhibiti wa Wanyama na Wadudu waharibifu kwa ya ajili ya tafiti na mafunzo. Jengo hilo limejengwa kwa ufadhili wa mradi wa Kituo cha Umahiri cha Afrika cha utafiti wa teknolojia za kunusa kwa kutumia panya kilichopo Kampasi Kuu. Mradi huu ni mmoja kati ya miradi miwili ambayo ni mkopo wa Serikali kutoka Benki ya Dunia na umegharimu kiasi cha shilingi Milioni 330. Matokeo ya utafiti huu yamekuwa ni msaada kwa sasa katika kubaini magonjwa yaliyokuwa yanachukua muda mrefu kugundulika kama vile kifua kikuu.

Picha chini ni muonekano wa jengo la kukuzia na kutunzia Wadudu na Wanyama wadogo waharibifu kwa ajili ya Utafiti

2.3 USHAURI WA KITAALAMU, HUDUMA ZA UGANI NA ATAMIZI.

Kuanzishwa kwa vituo vya huduma za ugani

Chuo kimeendelea kusambaza utaalamu, ubunifu, teknolojia na matokeo ya utafiti unaofanyika chuoni kupitia huduma ya ushauri wa kitaalamu na ugani. Kati ya mwaka 2015-2020, Chuo kimekuwa na vituo tisa (9) vya huduma za ugani katika mikoa ya Morogoro, Ruvuma, na Iringa. Katika eneo hili Chuo kimefanikiwa kuwafikia wakulima, wafugaji, wavuvi, mashirika ya serikali, mashirika binafsi na mashirika ya kimataifa. Ushauri huo umesaidia kutatua changamoto mbalimbali nchini hususan vijijini ambapo wakulima wanasaidiwa kuboresha shughuli zao za kilimo kwa kutumia mbinu za kisasa. Vilevile, Chuo kinatoa huduma za upimaji wa udongo, matumizi bora ya ardhi, upandaji miti, tiba kwa wanyamapori na mifugo, huduma za uhamilishaji kwa njia za kisasa, ushauri wa chakula na lishe na matumizi ya pembejeo na mbegu bora za kilimo.

Afisa Tawala Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emmanuel Kalobelo (mwenye mabuti) akikagua moja ya shamba wakati alipotembelea Mashamba darasa ya mfano yaliyopo Mlali wilaya ya Mvomero, Morogoro

Uanzishwaji wa kituo Atamizi cha mafunzo ya Kilimo-Biashara

Chuo kwa kushirikiana na Wakfu wa PASS kinaendesha mradi wa kulea na kufundisha vijana ujasiriamali kwenye sekta ya kilimo-biashara ili waweze kuongeza kipato chao na taifa kwa ujumla. Hadi kufikia mwezi Juni, 2020 miundombinu iliyojengwa kwenye Kituo Atamizi ni pamoja na vitalu-nyumba hamsini na mbili (52) na vingine hamsini (50) vinaendelea kujengwa, vitalu (20) vya mashamba kwa ajili ya kilimo cha nje (open field), miundo mbinu ya maji kwa ajili ya umwagiliaji, tanki kubwa la maji lenye ujazo wa lita laki moja (100,000), jengo litakalotumika kama soko la kuuzia mazao kwa waatamiwa na maandalizi ya ujenzi wa jengo la Utawala (Administration Block) yameanza.

Muonekano wa kituo Atamizi cha mafunzo ya Kilimo Biashara

Kati ya vitalu-nyumba hamsini na mbili (52) zilizopo sasa, mbili (02) zinatumika kwa ajili ya majaribio na arobaini na moja (41) ndizo zenye mazao ya waatamiwa katika mchanganuo ufuatao; nyanya nyumba vitalu mbili (02), tikitimaji nyumba-vitalu saba (07), tango nyumba-vitalu kumi na tano (15), pilipili hoho nyumba-vitalu kumi na tano (15) na maboga lishe nyumba-vitalu mbili (02).

Aidha, kazi ya kuunganisha umeme ipo katika hatua za mwisho kukamilika.

Vijana wanaoatamiwa hulelewa kwenye atamizi kwa muda wa mwaka mmoja na kupata ujuzi na weledi unaowawezesha kwenda kuanza kilimo-biashara katika maeneo mbalimbali nchini baada ya kuhitimu. Aidha, vijana hao hufundishwa kilimo cha mazao mbalimbali kwenye vitalu nyumba na maeneo ya wazi. Katika awamu ya kwanza waatamiwa 18 walifundishwa ambapo wahitimu 14 wapo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kupewa mikopo na benki ya maendeleo ya kilimo (TADB), mikopo hiyo inadhaminiwa na PASS kwa asilimia themanini (80%).

Awamu ya pili ina waatamiwa 49 wanaendelea kuatamiwa na wanatarajia kuhitimu mafunzo mwezi Disemba, 2020.

Baadhi ya wafanya biashara wakiwa kwenye soko lililopo kwenye kituo Atamizi cha mafunzo ya kilimo biashara

Muonekano wa shamba la matango lililopo kwenye kituo Atamizi cha mafunzo ya kilimo biashara



Vitalu-Nyumba vya mafunzo na utafiti

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa shilingi milioni 50 mwaka 2018 kwa ajili ya ujenzi wa vitalu-nyumba vipya vitatu chuoni. Vitalu-nyumba hivyo ni sehemu ya shamba darasa na hutumika kufanya tafiti na kufundishia wanafunzi na wakulima kuzalisha mazao. Chuo kina mpango madhubuti wa kuanzisha viwanda darasa vya mafunzo ya usindikaji mazao ya kilimo na mifugo ili kuwapa wanafunzi ujuzi na weledi utakaowawezesha kupata ajira kwenye viwanda au kujiajiri wenyewe mara baada ya kuhitimu.

Muonekano wa ndani wa moja ya Kitalu nyumba cha Mafunzo na Utafiti kilichopo Kampasi Kuu, SUA

Wanafunzi wakiwa kwenye mazoezi kwa vitendo katika shamba lililopo kwenye eneo la Vitalu-nyumba vya Mafunzo na Utafiti

3.0 HUDUMA KWA WANAFUNZI

Ujenzi wa dahalia kwenye mabweni ya Nicholaus Kuhanga

Kumekuwa na changamoto ya dahalia kwa ajili ya wanafunzi wanaoishi katika mabweni ya Nicholaus Kuhanga pamoja na wafanyakazi wa Shule Kuu ya Uchumi Kilimo na stadi za biashara. Hii ilipelekea wanafunzi na wafanyakazi kutembea umbali mrefu kupata huduma za chakula ambayo ilipelekea kuhatarisha usalama wao hususani nyakati za usiku. Serikali ya awamu ya tano kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika Mradi wa P4R ilitoa fedha kiasi cha shilingi milioni 700 zilizowezesha Ujenzi wa Dahalia yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 350 kwa wakati mmoja kwenye hosteli ya Nicholaus Kuhanga. Dahalia hii iliyokamilika mwezi Februari, 2019 imetatua na kupunguza changamoto ya awali ya kukosekana huduma bora ya chakula kwa wanafunzi na wafanyakazi.

Muonekano wa nje wa Dahalia iliyopo kwenye mabweni ya Nicholaus Kuhanga, picha ndogo ni muonekano wa ndani

Ukarabati wa mabweni ya wanafunzi

Ili kuboresha malazi ya wanafunzi, Chuo kimekarabati mabweni 6 likiwemo moja kwa ajili ya wanafunzi wa kigeni yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 882. Ukarabati huo umegharimu kiasi cha Shilingi Milioni 415.4. Ukarabati huo umehusisha vyoo na mabafu, kupaka rangi, kubadili nyavu za madirisha na vitasa vya milango na kurekebisha sehemu za paa zilizokuwa zinavuja. Lengo ni kuboresha malazi ya wanafunzi ili kuendelea kuvutia wanafunzi wanaokuja kusoma SUA kutoka ndani na nje ya nchi. Chuo kitaendelea na ukarabati wa mabweni mengine ya wanafunzi kulingana na upatikanaji wa fedha.

Muonekano wa moja ya Mabweni ya wanafunzi ambayo yamefanyiwa ukarabati

Muonekano wa bweni kwa ajili ya wanafunzi wa kigeni

Ununuzi wa mabasi ya kusafirisha wanafunzi

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kina Kampasi mbili mjini Morogoro hivyo baadhi ya wanafunzi hulazimika kuwa na vipindi katika Kampasi zote mbili kwa nyakati tofauti.

Kwa muda mrefu Chuo kimekuwa kikitumia mabasi mawili tu yaliyokuwa yanahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Katika kutatua changamoto hiyo Chuo kimenunua mabasi mawili aina ya TATA kwa gharama ya shilingi Milioni 406. yenye uwezo wa kubeba abiria 61 kila moja. Mabasi haya kwa kiasi kikubwa yamepunguza changamoto ya usafiri kwa wanafunzi kati ya kampasi hizi mbili na kwenda kwenye vituo vya mafunzo nje ya mji wa Morogoro.

Muonekano wa basi la zamani la kusafirishia wanafunzi

Muonekano wa basi jipya kwa ajili ya kusafirishia wanafunzi

3.1 MABORESHO YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA MTAMBUKA

Ukarabati wa majengo ya Ndaki ya Sayansi na Tiba za Wanyama

Chuo kimepatiwa kiasi cha shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa majengo ya Ndaki ya Sayansi na Tiba za Wanyama. Ukarabati huo utajumuisha ofisi, madarasa, maabara na upanuzi wa hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama, miundombinu chakavu ikiwemo maabara, mashine za kuhifadhia mizoga ya kufundishia na uchunguzi wa magonjwa vimerekebishwa. Pia ukarabati huu unahusisha majengo na malisho ya Wanyama yaliyopo kwenye shamba la mafunzo la mfano kitengo cha magadu.

Picha kubwa ni Muonekano wa Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya wanyama ambayo inaendelea kufanyiwa ukarabati. Picha ndogo ni muonekano wa majengo mengine ya Ndaki ya Sayansi na Tiba za Wanyama yanayoendelea kukarabatiwa

Ukarabati wa majengo na ununuzi wa vifaa vya ofisi

Hali ya majengo mengi ya SUA ilikuwa sio ya kuvutia kwa uchakavu lakini pia baadhi ya majengo yalikuwa yanahatarisha maisha ya wanajumuiya kwa kuwa na nyufa. Aidha kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto ya vifaa vya Ofisi hususan viti vya kukalia.

Katika kipindi cha mwaka 2015-2020, Chuo kimefanya ukarabati wa majengo ya ofisi mbalimbali ikiwemo Jengo Kuu la Utawala kwa gharama ya shilingi milioni 95.4, jengo la Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza shilingi milioni 91.2, kituo cha Askari Wasaidizi wa SUA shilingi milioni 77.6, jengo la Idara ya Sayansi za Wanyama shilingi milioni 92.5. Majengo mengine yaliyokarabatiwa ni pamoja na jengo la Ndaki ya Kilimo pamoja na jengo la Idara ya Kilimo Ugani na Maendeleo ya Jamii. Ukarabati huo umehusisha kupaka rangi, kubadili paa, kubadili nyavu za madirisha, kuweka marumaru na kurekebisha eneo la maegesho na mandhari ya jengo la Utawala. Chuo kitaendelea na ukarabati wa ofisi za wafanyakazi kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Chuo kimenunua jumla ya viti 230 vyenye thamani ya shilingi milioni 39.

Muonekano wa Jengo Kuu la Utawala lililopo Kampasi Kuu baada ya kufanyiwa ukarabati. Picha ndogo ni muonekano wa jengo hilo kabla ya ukarabati

Muonekano wa Jengo Elimu ya Kujiendeleza (ICE) baada ya kukarabatiwa. Picha ndogo ni muonekano wa jengo hilo kabla ya ukarabati

Muonekano wa Jengo la kituo cha askari wasaidizi SUA. Picha ndogo ni muonekano wa kituo hicho kabla ya kukarabatiwa

Ukarabati wa barabara

Chuo kinakarabati barabara za Kampasi ya Solomon Mahlangu kuanzia getini hadi utawala (mita 916) na barabara za Kampasi kuu (km 1.3) imekarabatiwa kwa gharama ya shilingi milioni 780, mapato ya ndani. Ujenzi huu utarahisisha usafiri kwa wanafunzi na wanajumuiya yote ya SUA kufika kwa urahisi sehemu mbalimbali za Chuo.

Muonekano wa moja ya barabara ya Kampasi Kuu kabla ya kufanyiwa ukarabati

Muonekano wa moja ya barabara ya Kampasi Kuu baada ya kufanyiwa ukarabati

Muonekano wa barabara ya Kampasi ya Solomon Mahlangu kabla ya kufanyiwa ukarabati

Muonekano wa barabara ya Kampasi ya Solomon Mahlangu baada ya kufanyiwa ukarabati

Upanuzi wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

SUA imepanua hospitali yake kwa kujenga wodi mbili zenye uwezo wa kulaza wagonjwa 40 na kununua vifaa vya uchunguzi ikiwa ni pamoja na mashine ya kisasa ya "X-ray" kwa gharama ya shilingi Milioni 346.1 na kuboresha Kitengo cha Huduma ya Tiba ya meno kwa kununua vifaa tiba vipya kwa gharama ya shilingi Milioni 41.1. Vifaa hivyo vimesaidia kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii inayokizunguka Chuo na Mkoa wa Morogoro kwa ujumla. Hospitali hii imesajiliwa na kupewa hadhi ya Hospitali ya Wilaya kwa mujibu wa vigezo vya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Muonekano wa Hospitali ya SUA baada ya kufanyiwa upanuzi. Picha ndogo ni muonekano wa vifaa vya tiba ya kinywa

Ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo

Menejimenti ya Chuo imechukua hatua za makusudi kuboresha miundombinu ya michezo chuoni ikiwa ni pamoja kujenga uwanja mpya na wa kisasa wa mpira wa kikapu na kuchimba mitaro mikubwa pembeni mwa viwanja ili kutengeneza mikondo ya maji kuzuia maji kujaa uwanjani. Ujenzi huo umegharimu kiasi cha shilingi Milioni 54.2 Chuo kina lengo la kuendelea kuboresha miundombinu ya michezo kwa kujenga miundombinu mipya, kutunza na kukarabati miundombinu iliyopo ili kuendeleza michezo chuoni.

Picha kubwa ni muonekaano wa kiwanja cha mpira wa kikapu baada ya kukarabatiwa. Picha ndogo ni muonekano wa awali wa kiwanja hicho

HUDUMA ZA BIASHARA

Ujenzi wa vibanda vya biashara chuoni

Wanajumuiya wa SUA walikuwa wakilazimika kwenda Morogoro-mjini kupata mahitaji madogo madogo. Ili kusogeza huduma hizo muhimu kwa wanafunzi na Wafanyakazi, Chuo kimejenga viban-da vya kisasa vya biashara (maduka) kwa ajili ya kutoa huduma za bidhaa muhimu za kijamii ndani ya eneo la Chuo. Jumla ya vibanda 18 vya biashara vimejengwa sehemu moja kwa ajili ya uuzaji wa mahi-taji mbalimbali kwa wanafunzi na wanajumuiya wa SUA. Gharama za ujenzi wa vibanda hivyo ni shilingi Milioni 142.1

Picha kubwa ni muonekano wa vibanda vipya vya biashara kwa ajili ya Wanajumuiya wa SUA., Picha ndogo ni muonekano wa vibanda vya zamani

HUDUMA ZA KIBENKI

Chuo kimeimarisha huduma za Kibenki kwa wanajumuiya ambapo Benki ya CRDB ina matawi katika Kampasi zote mbili za Chuo na kwa sasa Benki ya NMB imefungua Tawi dogo Kampasi Kuu kwa ajili ya kutoa huduma za kibenki. Uwepo wa huduma hizi umeweza kusaidia wanajumuiya ya Chuo kupata huduma za kibenki kwa urahisi kwa wakati.

Picha juu ni jengo lenye tawi la benki ya CRDB na chini ni muonekano wa tawi dogo la benki ya NMB

3.2 VYANZO VYA MAPATO YA CHUO

Chuo kinategemea vyanzo vya mapato mbalimbali kutoka Serikalilini, kwa Wadau wa Maendeleo pamoja na mapato ya ndani ili kujiendesha. Ufuatao ni Mchanganuo wa Fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya Chuo.

RUZUKU KUTOKA SERIKALINI (MISHAHARA NA MARUPURUPU)

Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, Chuo kilipokea jumla ya shilingi bilioni 74.5 kutoka serikali kuu kwa ajili ya mishahara na marupurupu.

FEDHA ZA MAENDELEO

Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2016 hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, Chuo kilipokea jumla ya shilingi bilioni 11.4 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

FEDHA ZA MIRADI YA UTAFITI KUTOKA WADAU WA MAENDELEO

Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2016 hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, Chuo kilipokea fedha kwa ajili ya shughuli za utafiti kutoka kwa wadau wa maendeleo kiasi cha Shillingi 60,277,149,901.32. Fedha zimesaidia kutekeleza shughuli mbalimbali za utafiti na kusaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hususani ujenzi wa miundo mbinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

MAPATO YA NDANI

Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2016 hadi kufikia Mwezi Machi, 2019 Chuo kimefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi 54,791,700,323.10 kutokana na mapato ya ndani ya Chuo kutoka vyanzo mbambali vya mapato chuoni. Shughuli hizo ni pamoja na ufundishaji, ukodishwaji wa majengo ya Chuo na vitengo vingine vya uzalishaji mali. Chuo pia kimefanikiwa kutenga Kiasi cha Shillingi bilioni 3.8 kutoka kwenye vyanzo vyake mbambali vya mapato ya ndani kwa ajili ya shughuli za maendeleo .

Aidha, mapato ya ndani yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kudhibiti ukusanyaji mapato kwa kutumia mashine za

TEUZI ZA RAIS

Katika kipindi cha Mwaka 2015 hadi 2020 Mhe. Rais amefanya teuzi mbalimbali za watumishi kutoka SUA kwenda kushika nafasi za uongozi kwenye Wizara, Taasisi pamoja na Mashirika mbalimbali ya Umma. Hii inaonesha dhahiri uaminifu wake kwa Chuo hiki na kukifanya kizidi kujitangaza ndani na nje ya nchi. Teuzi hizo zinaonekana katika jedwari hapa chini;

JINA	NAFASI	MAHALI	KIPINDI
Prof. Raphael T. Chibunda	Mwenyekiti wa Bodi	Shirika la Elimu Kibaha	Kuanzia tarehe 14 Februari, 2020
Prof. Hamis O. Dihenga	Mjumbe na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Saratani	Ocean Road	kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 22 Oktoba 2015 hadi tarehe 21 Oktoba 2018.
Prof. (Mrs.) Salome K. Mutayoba	Mwenyekiti wa Bodi	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)	Miaka mitatu kuanzia tarehe 01.09.2015 hadi tarehe 02.09.2018.

JINA	NAFASI	MAHALI	KIPINDI
Prof. Damian Gabaghambi	Mkurugenzi	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)	Kuanzia tarehe 22 Machi, 2018.
Prof. Carolyne I. Nombo	Mwenyekiti wa Bodi	Shirika la Masoko Kariakoo	Miaka mitatu kuanzia tarehe 23 Aprili, 2018.
Prof. Romanus C. Ishengoma	Mwenyekiti wa Bodi	Mifuko ya Misitu Tanzania;	
Prof. Joyce L. D. Kinabo	Mwenyekiti wa Bodi	Taasisi ya Chakula na Lishe, Tanzania.	
Prof. Sebastian Wilson Chenyambuga	Mwenyekiti wa Bodi	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)	Kuanzia tarehe 26 Januari, 2019
Prof. Frederick Cassian Kahimba	Mkurugenzi Mkuu	Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO)	Kuanzia tarehe 31 Agosti, 2019.

3.3 HITIMISHO

Chuo Kikuu cha Sokoine kimepiga hatua kubwa katika kufikia mpango mkakati wake wa miaka mitano kufuatia kuboreshwa kwa miundombinu na mifumo mbalimbali. Haya yote yamewezekana kutokana na mchango mkubwa ambao Chuo kimepata kutokana na maono makubwa ya Mhe.Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kuendeleza Elimu. Chuo kitaendelea kuomba msaada zaidi wa Serikali ili kutimiza malengo yake na kuwa chachu katika kujenga uchumi wa viwanda.

IMETOLEWA NA:

OFISI YA MAWASILIANO NA MASOKO
S.L.P. 3000 CHUO KIKUU,
MOROGORO, TANZANIA
Simu: 255-023-2640006/7/8/9,
Barua pepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz

www.sua.ac.tz

MIAKA MITANO YA JPM